Hima tujenge nyumba moja!

Watanzania wanasemaje kuhusu Jumuiya ya Afrika Mashariki

1. Utangulizi

Mnamo Julai 2000, Jumuiya ya Afrika Mashariki ilianzishwa kwa njia ya makubaliano kati ya Tanzania, Kenya na Uganda. Hizi nchi tatu zilianzisha Shirikisho lililotiwa saini mwaka 1967. Rwanda na Burundi zilijiunga Julai 2007. Umoja wa Hiari ulikuja 2005, ukaanzisha ushuru wa pamoja na biashara huru ya pamoja kwa nchi wanachama. Soko la Pamoja lilianza tarehe 1 Julai 2010. Hili lilifungua milango minne ("uhuru wa aina nne"), ikimaanisha: mzunguko huru wa bidhaa; wafanyakazi; huduma; na fedha. Hii ililenga kwa kiasi kikubwa kukuza biashara na uwekezaji na kufanya eneo hili liongeze uzalishaji na utajiri/tija[1].

Maoni ya wananchi yamechangia kwa kiasi kikubwa katika historia ya hivi karibuni ya Tanzania ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Utafiti wa *Afrobarometer* uliofanyika 2007-08[2] uligundua kuwa idadi kubwa ya wananchi walipendelea ushirikiano wa kiuchumi na siyo ushirikiano wa kisiasa. Matokeo haya ni moja kati ya hoja zilizotumiwa na Tanzania kutojiunga na wanachama wengine watatu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki katika kile kinachojulikana kama Ushirikiano wa Hiari (Coalition of the Willing [COW]) ambao wanaongeza kasi ya kufikia ushirikiano wa kikanda. Mikutano kadhaa ya COW ya mwaka 2013 iliainisha majukumu maalumu ya kila nchi katika ajenda ya kuharakisha ushirikiano. Kwa mujibu wa gazeti la *"The East African"* (31 Agosti 2013) "Kenya inaongoza katika ufuaji na usambazaji wa mabomba na umeme; Rwanda katika Umoja, visa ya pekee na vitambulisho vya Jumuiya ya Afrika Mashariki; na Uganda katika reli na shirikisho la kisiasa".

[1] http://www.eac.int/commonmarket/

[2] Katera, Lucas (2009). Citizens' views on the East African Federation: a Tanzanian perspective. Afrobarometer Briefing Paper, REPOA, Dar es Salaam.

Muhtasari huu umeandaliwa na Twaweza, iliyopo Hivos Tanzania kwa ushirikiano na *Society for International Development.* Wachangiaji ni Angela Ambroz, Aidan Eyakuze, Evarist Kamwaga, Elvis Mushi, Youdi Schipper na Tunu Yongolo.

Takwimu zilikusanywa na Ipsos Tanzania. Imetolewa Oktoba 2014.

SID
Society for International Development

Twaweza ni sisi

S.L.P. 38342, Dar es Salaam, Tanzania.
Simu: +255 22 266 4301 | barua pepe: uwazi@twaweza.org | www.twaweza.org/sauti

Kuwepo kwa vipengele hivi katika ajenda ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kunaweza kuwa na athari kubwa katika maisha ya watu na biashara. Je, Watanzania wanaufahamu gani kuhusu ajenda na mapendekezo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki? Je, wanakubaliana na mapendekezo haya? Ni nini maana ya mapendekezo haya? Na je, Tanzania itaongoza, itapunguza mwendo au itajitoa kabisa katika ushirikiano huu wa kikanda?

Muhtasari huu unatoa takwimu juu ya mitazamo ya wananchi kuhusu mchakato unaoendelea wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Takwimu hizi zinatoka katika Awamu ya 23 ya Sauti za Wananchi, utafiti wa kwanza wenye uwakilishi wa kitaifa barani Afrika uliofanywa kwa njia ya simu za mkononi (www.twaweza.org/sauti). Takwimu zilikusanywa kwa kushirikiana na *Society for International Development* na zilijumuisha washiriki 1,408 kutoka Tanzania Bara. Simu zilipigwa kati ya tarehe 13 hadi 22 Agosti, 2014.

Matokeo muhimu ya muhtasari huu ni:

- Wananchi wanane kati ya kumi wanaamini kuwa tunapaswa kubaki mwanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.
- Watanzania wawili kati ya watatu ambao wanafahamu kuhusu Umoja wa Hiari (COW) wanataka kuwa sehemu ya Umoja huo.
- Kenya na Uganda ni washirika pendwa wa ushirikiano kwa Watanzania.
- Mambo yanayopendwa kuliko yote katika ushirikiano ni visa ya pekee ya utalii katika kanda, kusafiri ndani ya Afrika Mashariki kwa kutumia vitambulisho vya taifa, na miradi ya pamoja ya miundombinu. Wananchi wanane kati ya kumi wanaunga mkono mambo haya.
- Watanzania saba kati ya kumi wanaunga mkono mzunguko huru wa wafanyakazi ndani ya Afrika Mashariki na uwepo wa pasi ya kusafiria moja kwa nchi zote.

2. Mambo saba kuhusu maoni ya Wananchi juu ya Jumuiya ya Afrika Mashariki

Jambo la 1: Watanzania sita kati ya kumi (58%) wanatambua uwepo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki

Kwa wale waliowahi kusikia kuhusu Afrika Mashariki, tuliwaomba waelezee kwa maoni yao kuwa ni aina gani ya ushirikiano ambao waliamini Jumuiya ya Afrika Mashariki inalenga. Miongoni mwa washiriki hao, 65% walijibu kuwa ni wa kiuchumi, na vikundi vya wachache vikiamini kuwa ni wa kijamii (17%) au wa kisiasa (12%) (Kielelezo 1). Ikumbukwe kuwa lengo la Jumuiya ya Afrika Mashariki ni muungano wa kisiasa katika muundo wa shirikisho.

Kielelezo cha 1: Aina ya ushirikiano
(kati ya wale waliosikia kuhusu Jumuiya ya Afrika Mashariki)



Chanzo cha takwimu: *Sauti za Wananchi* - Awamu ya 23, Agosti 2014.

Jambo la 2: Watanzania wengi wanaona athari chanya za Jumuiya ya Afrika Mashariki

Tuliwauliza Watanzania iwapo walidhani athari ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa uchumi, usalama, siasa, na utamaduni wa Tanzania utakuwa chanya au hasi. Katika maeneo haya yote, Watanzania walionesha kutarajia athari chanya kuliko athari hasi (Kielelezo 2). Kwa mfano, wananchi zaidi ya mara mbili walitarajia athari chanya za kiuchumi kuliko wale ambao waliohofu kuwa ushirikiano utakuwa na madhara ya kiuchumi (42% dhidi ya 20%).

Kielelezo cha 2: Unafikiri athari ya Jumuiya ya Afrika Mashariki itakuwa nini kwa Tanzania?



Chanzo cha takwimu: *Sauti za Wananchi* - Awamu ya 23, Agosti 2014.

Jambo la 3: Kati ya wanachama wote, Kenya na Uganda ni washirika pendwa

Tofauti na simulizi za kawaida za uhasama kati Tanzania na Kenya, bado Kenya ni moja kati ya washirika pendwa wa ushirikiano kati ya nchi zote jirani: 85% ya Watanzania wamesema kuwa ama “wanakubali sana” au “wanakubali” ushirikiano na Kenya (Kielelezo 3). Uganda ni vivyo hivyo (Kielelezo 3).

Nchi ambayo inakubalika kwa kiwango cha chini kabisa ni Sudan ya Kusini: 44% tu ya Watanzania wameonesha kukubali ushirikiano na nchi hii (Kielelezo 3).

Kielelezo cha 3: Ni kwa kiwango gani unachokubali/ kutokukubaliushirikiano wa Tanzania na…



Chanzo cha takwimu: *Sauti za Wananchi* - Awamu ya 23, Agosti 2014.

Jambo la 4: Wananchi wengi wanaunga mkono kuharakisha kasi ya ushirikiano

Watanzania wanane kati ya kumi (80%) walikuwa hawajawahi kusikia kuhusu “Umoja wa Hiari” (takwimu hazijaoneshwa). Tuliwaelezea kwa ufupi kuwa nchi hizi tatu (Kenya, Rwanda na Uganda), walikubaliana kuharakisha michakato ya ushirikiano katika miundombinu, na baadhi ya masuala ya uhamiaji na ya kisiasa; na kuwa Tanzania si sehemu ya kundi hili.

Wananchi waliokuwemo katika kundi la wale wasiowafahamu kuhusu Umoja huu waliulizwa iwapo Tanzania (na Burundi) ijiunge, majibu yao yalikuwa yamegawanyika (Kielelezo 4). Hata hivyo, washiriki ambao walifahamu makubaliano hayo walikuwa na maoni chanya: 67% ya kundi hili waliamini kuwa Tanzania inapaswa kuwa mshiriki, dhidi ya 28% ambao hawakutaka ijiunge.

Kielelezo cha 4: Ni kwa kiasi gani unakubaliana na kauli hii, "Tanzania (na Burundi) zinapaswa kuwa sehemu ya Umoja wa Hiari"?



Chanzo cha takwimu: *Sauti za Wananchi* - Awamu ya 23, Agosti 2014.

Jambo la 5: Vipengele vinavyopendwa zaidi katika Jumuiya ya Afrika Mashariki ni visa ya pekee na kitambulisho cha kitaifa cha kusafiria

Tuliwaeleza washiriki sifa kuu za Shirikisho la Afrika Mashariki lililopendekezwa. Hizi zilikuwa pamoja na ushirikiano wa kiuchumi na wa kisiasa ambao unaweza kuleta matokeo muhimu katika maisha ya watu ya kila siku. Jambo la kushangaza lilikuwa, vipengele vilivyopendwa kuliko vyote vya Shirikisho ni (1) kuanzishwa kwa visa ya pekee ya utalii kuwezesha wageni kutembelea nchi yoyote katika Afrika Mashariki (82% ya Watanzania walilikubali hili), na (2) uwezo wa wananchi wa Afrika Mashariki kusafiri nchi yoyote ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa kutumia kitambulisho kimoja tu cha kitaifa (82%) (Kielelezo 5). Mapendekezo mengine muhimu yaliyokubaliwa na wengi ni mzunguko huru wa wafanyakazi ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki; miradi ya pamoja ya miundombinu; na kuanzishwa kwa pasi ya kusafiria moja kwa nchi zote.

Jambo la kuvutia ni kukubalika kwa baadhi ya mapendekezo haya. Mzunguko huru wa wafanyakazi ulikubalika kwa 69% katika utafiti wa Sauti za Wananchi 2014 na mzunguko huru wa watu, bidhaa na huduma ulikubalika kwa 67% mwaka 2008 (REPOA). Ingawa Soko la Pamoja limekuwapo tangu 2010, mzunguko huru kwa wafanyakazi bado haujatengamaa. Hii inaoonekana hapo wafanyakazi wasio na vibali wanapofukuzwa mara kwa mara Tanzania wakitoka nchi zingine.

Mapendekezo yanayokubalika kwa kiwango cha chini kabisa ni: kuundwa kwa jeshi la pamoja (64% wanakataa), kuruhusu umiliki wa ardhi kwa wananchi wa Afrika Mashariki katika nchi nyingine za Jumuiya (70% wanakataa), na Serikali ya pamoja yenye Bunge moja la wanachama (71% wanakataa) (Kielelezo 5).

Kielelezo cha 5: Ngazi ya ukubali wa kila vipengele vya Jumuiya ya Afrika Mashariki



Chanzo cha takwimu: *Sauti za Wananchi* - Awamu ya 23, Agosti 2014.

Jambo la 6: Watanzania wanane kati ya kumi wanaamini tunapaswa kuwa katika Jumuiya ya Afrika Mashariki

Kwa ujumla, Watanzania wana matumaini na Jumuiya ya Afrika Mashariki na uwezo wake wa kuleta faida kwa nchi. Wananchi wanane kati ya kumi (80%) waliamini Tanzania haipaswi kujiondoa katika Jumuiya ya Afrika Mashariki (Kielelezo 6).

Pamoja na matumaini hayo, tulipowauliza wataje fursa kuu tatu kwa Tanzania, ni 12% tu waliotaja “biashara “ kama mojawapo. (Majibu pendwa kuliko yote kwa swali hili yalikuwa utalii (57%) na uchimbaji wa madini (57%) takwimu hazijaonyeshwa).

Kielelezo cha 6: Je, Tanzania ijiondoe katika Jumuiya ya Afrika Mashariki?



Chanzo cha takwimu: *Sauti za Wananchi* - Awamu ya 23, Agosti 2014.

Jambo la 7: Watanzania wana matumaini ya kudumu kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki

Walipoulizwa kuhusu jinsi wao wanavyoiona Jumuiya ya Afrika Mashariki katika miaka kumi ijayo, (yaani, mwaka 2025), Watanzania wengi walikuwa na matumaini mengi: walifikiri kuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki itakuwa imara, na Tanzania itabaki kuwa mwanachama wa muhimu (Kielelezo 7). Theluthi mbili ya Watanzania wanaona mustakabali wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ukiwa "wenye nguvu" au "sawa na leo", lakini 25% ya washiriki hawakuwa na uhakika wa nini cha kutarajia.

Kielelezo cha 7: Je, ndani ya miaka kumi ijayo, Jumuiya ya Afrika Mashariki itakuwapo?



Chanzo cha takwimu: *Sauti za Wananchi* - Awamu ya 23, Agosti 2014.

3. Hitimisho

Watanzania wengi wanafahamu kuhusu Jumuiya ya Afrika Mashariki na wanao uelewa dhahiri kuhusu jambo hilo. Vichwa vya habari katika toleo la utafiti wa Sauti za Wananchi uliofanywa mwezi Agosti 2014 na shirika la Twaweza kupitia simu ya mkononi kuhusu Jumuiya ya Afrika Mashariki yalionesha kuwa:

- Watanzania wana maoni chanya kuhusu Jumuiya ya Afrika Mashariki, fursa za kiuchumi zitakazotokana nayo na athari zake.
- Watanzania hawaungi mkono kuundwa kwa jeshi la pamoja la Afrika Mashariki au Serikali moja - lakini wanaunga mkono ushirikiano katika utawala na pasi ya kusafiria ya pamoja, pia uwezo wa kusafiri kwa vitambulisho vya kitaifa na mzunguko huru wa wafanyakazi ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.
- Wakiangalia mbele kwenda mwaka 2025, theluthi mbili ya Watanzania wanaona Jumuiya ya Afrika Mashariki ikiwa imara kama ilivyo sasa, au hata imara zaidi.

Pia wengi wana mtazamo chanya kuhusu ushirikiano na nchi za Kenya na Uganda zenye uchumi mkubwa katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Idadi kubwa ya Watanzania (80%) hawafahamu uwepo wa Ushirikiano wa Hiari (mijadala mikali kote): miongoni mwa wale ambao wanafahamu kuhusu Umoja huo, 67% wangependa Tanzania ishiriki.

Kuhusu masuala mengine muhimu, walio wengi wanakubali kuanzishwa kwa uwezo wa wananchi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kusafiri popote katika nchi wanachama kwa kutumia tu vitambulisho vyao vya kitaifa. Zaidi ya hayo, wengi wanakubali miradi ya pamoja ya miundombinu inayovuka mipaka na mzunguko huru wa wafanyakazi.

Hivi vipengele ni vya msingi na vinaashiria faida kubwa na endelevu ya kiuchumi kwa Watanzania wote kwa pamoja na kwa mtu mmoja mmoja. Kuondoa vikwazo vya watu kuvuka mipaka kutasaidia wafanyakazi na watalii. Katika soko huru la ndani la ajira, wafanyakazi huruhusiwa kutumia vipaji vyao popote katika Jumuiya ya Afrika Mashariki bila vibali vya gharama ambavyo kwa sasa mara nyingi huhitajika. Hii italeta faida mbili: moja kwa Watanzania ambao wataweza kupata kazi, kwa mfano, katika nchi za Rwanda au Kenya na pili; kwa Watanzania ambao watapata huduma – mfano masomo ya Kiingereza kwa watoto wao - yatakayotolewa na Wakenya, Waganda na wananchi wengine wa Jumuiya ya Afrika Mashariki nchini Tanzania.

Hoja hii ya mwisho mara nyingi husahauliwa katika majadiliano kuhusu vibali vya kazi (na wahamiaji haramu). Moja ya faida kubwa la soko la ajira la Jumuiya ya Afrika Mashariki ipo kwa upande wa mahitaji: raia wa Tanzania wanaweza kunufaika na ongezeko la kuenea kwa vipaji. Hii faida ni ya papo kwa hapo na pia ina nguvu ya kuboresha usambazaji kuendeleza ushindani mkubwa katika huduma na kujifunza mustakabali wa mbali.

Faida nyingine za Jumuiya ya Afrika Mashariki ni kama vile uwekezaji wa pamoja katika miundombinu kati ya nchi na nchi ambayo itawaruhusu wauzaji wa Tanzania kuuza bidhaa katika nchi za nje kwa gharama za chini ili kuongeza ushindani. Taarifa juu ya "The drivers of economic growth and poverty reduction in Africa", chapisho lililoharirwa na Profesa Benno Ndulu, Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, inasema: "Kwa upande wa biashara, ushahidi unaonyesha kuwa ushirikiano na masoko ya kimataifa unahusishwa na ukuaji, uimarishaji wa mikakati ya ukuaji ili kusisitiza na kuongeza aina mbalimbali za mauzo ya nje. Kuimarisha ushindani na kupunguza vikwazo vya biashara ni maeneo mawili muhimu ya kutekeleza hayo."[3]

Wananchi wanakubaliana na wataalamu kuhusu faida za kiuchumi zinazotokana na Jumuiya ya Afrika Mashariki. Hata hivyo, kuna hatari ya kupoteza fursa ambazo ni sehemu ya hali ya msukumo wa sasa wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kwa ustawi wa kizazi cha sasa na cha siku zijazo, ni wazi Tanzania haiwezi kumudu kukosa manufaa hayo ya ukuaji wa uchumi unaotokana na ushirikiano zaidi. Wakati umefika wa wanadiplomasia wa uchumi wa Tanzania kulinda na kuimarisha fursa hizi ili wananchi wao waweze kuzifurahia.

[3] Ndulu, Benno, Lopamudra Chakraborti, Lebohang Lijane, Vijaya Ramachandran, and Jerome Wolgin (2007). *Challenges of African Growth: opportunities, constraints and strategic directions. World Bank, Washington.*